

Waganga Wakuu wa mikoa na wilaya au kituo chochote cha polisi kilicho karibu naye. Aidha mwananchi anaweza kuwasiliana na Mamlaka kuitia simu bila malipo namba **0800110084**.


## 7. Changamoto za kupambana na dawa bandia

TMDA inakabiliana na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

- Ukubwa wa nchi na uwepo wa mipaka isiyo rasmi
- Uwepo wa wafanyabiashara wenyewe tamaa ya kupata faida haraka bila kujali afya ya jamii.
- Uelewa wa watumiaji/wananchi kuhusu dawa bandia

## 8. Wito

TMDA inatoa wito kwa wananchi kuwa makini wakati wanunua dawa na kuzichunguza vizuri kabla ya kuzitumia. Vilevile, pale watakobaini au kuhisi dawa yoyote kuwa bandia basi watoe taarifa mapema ili hatua za haraka ziweze kuchukuliwa.



### Mkurugenzi Mkuu,

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA),  
S.L.P 1253 Dodoma au 77150 Dar es salaam.  
Simu+255 22 2450512/2450751/2452108

Barua pepe: [info@tmda.go.tz](mailto:info@tmda.go.tz)

Tovuti: [www.tmda.go.tz](http://www.tmda.go.tz)

**Simu bila malipo: 0800110084**



### Kanda ya Ziwa

Barabara ya Nyasaka,  
Nyakato Buzuruga,  
S.L.P 543,  
Ilemela - Mwanza  
Simu +255 28 2981224/5  
Barua pepe: [info.mwanza@tmda.go.tz](mailto:info.mwanza@tmda.go.tz)

### Kanda ya Mashariki

Jengo la GEPF,  
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,  
S.L.P 31356,  
Dar es salaam,  
Simu +255 739 226328/788470312  
Barua pepe: [info.easternzone@tmda.go.tz](mailto:info.easternzone@tmda.go.tz)

### Kanda ya Kati

S.L.P 1253 Dodoma.  
Simu +255 26 2320156  
Barua pepe: [info.dodoma@tmda.go.tz](mailto:info.dodoma@tmda.go.tz)

### Kanda ya Magharibi

Jengo la TUWASA,  
S.L.P 520, Tabora  
Simu +255 262606082  
Barua pepe: [info.tabora@tmda.go.tz](mailto:info.tabora@tmda.go.tz)

## MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA



Tanzania Medicines & Medical Device Authority



## UDHIBITI WA DAWA

## BANDIA

**TMDA - Hulinda Afya ya Jamii**

## **1. Utangulizi**

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ni taasisi ya Serikali iliyo chini ya Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto yenye jukumu la kulinda afya ya jamii dhidi ya matumizi ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi. Pamoja na majukumu mengine, Mamlaka ina wajibu pia wa kupambana na dawa bandia na duni zilizoko katika soko.

## **2. Maana ya dawa bandia**

Dawa bandia ni dawa zilizotengenezwa kwa makusudi ya kudanganya au kuficha uhalisia wake kwa njia ya vifungashio, lebo au/na viambata vinavyotumika. Dawa hizi zinaweza kutokuwa na kiambata hai, kuwa na kiambata chini ya kiwango au kuwa kwenye kifungashio ambacho si chake kwa lengo la kupata faida isivyo halali.

## **3. Sababu za uwepo wa dawa bandia**

Dawa bandia ni tatizo la dunia nzima ikiwemo Tanzania. Uwepo wa dawa bandia kwenye soko la Tanzania unatokana na sababu zifuatazo:

- Kuwepo kwa waagizaji na usambazaji wasio waaminifu wanaojali maslai yao kuliko afya za walaji
- Mahitaji makubwa ya dawa kuzidi uwezo wa utengenezaji au usambazaji
- Bei kubwa ya dawa katika soko
- Kukua kwa sayansi na teknolojia na hivyo kusababisha kuiga na kutengeneza dawa kwa urahisi

- Kutokuwepo na ushirikiano mzuri baina ya wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na wasimamizi wa sheria
- Kutokuwa na mfumo madhubuti wa udhibiti wa dawa kwenye nchi jirani
- Uelewa mdogo wa wananchi / wadau kuhusu dawa bandia



## **4. Madhara ya dawa bandia**

Dawa bandia husababisha madhara yafuatayo:

- Wagonjwa kutokupona pale wanapotumia dawa na hivyo huweza kusababisha vifo
- Wagonjwa kupata madhara mbalimbali ya dawa
- Kupunguza uaminifu kwenye mfumo mzima wa utoaji huduma za afya ikiwa ni pamoja na wataalamu wa afya
- Kupunguza sifa, imani au umaarufu wa viwanda vya dawa ambavyo dawa zake zimeigizwa
- Kupunguza ukuaji wa viwanda vya dawa vya ndani ya nchi
- Kushuka kwa uchumi wa nchi

## **5. Majukumu ya TMDA katika kupambana na dawa bandia**

TMDA imekuwa mstari wa mbele katika kupambana na dawa bandia nchini. Mambo ambayo yamekuwa yakifanyika na yanaendelea kufanyika hadi sasa ni pamoja na:

- Kutengeneza miongozo ya kupambana na dawa bandia
- Kufundisha wakaguzi jinsi ya kupambana na dawa bandia
- Kutathmini na kusajili dawa kabla ya kuruhusu kuingia sokoni
- Kusajili na kutoa vibali vya utengenezaji, uingizaji, usambazaji na uuzaaji wa dawa
- Kuchunguza dawa kwenye maabara kabla na baada ya usajili
- Kufanya ukaguzi kwenye vituo vya forodha, maduka ya dawa pamoja na maeneo yote yanayohusika na usambazaji au uuzaaji wa dawa
- Kutoa adhabu kwa wale wanaokiuka sheria na kukutwa wanafanya biashara ya dawa bandia kwa mujibu wa sheria
- Kukuza ushirikiano baina ya taasisi mbalimbali hususani wasimamizi wa sheria kama TRA, Polisi n.k

## **6. Jinsi ya kutoa taarifa juu ya uwepo wa dawa bandia**

Iwapo mwananchi atabaini au kuhisi uwepo wa dawa bandia kwenye soko atoe taarifa na/au awasilishe dawa anayohisi kuwa bandia katika ofisi za TMDA, ofisi za